**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

**Simu/Fax : +255 232935205**
Barua pepe : dakawatc@moe.go.tz

Chuo Cha Ualimu Dakawa
S. L. P. 944
**MOROGORO.**

**Kumb. Na.** ***DKWTC/JSTR/VOL.1/***

**Tarehe 30/05/2025**

**Ndugu………………………………………………………..……**
**S.L.P. ……………………………………………….…………..**

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA STASHAHADA YA UALIMU ELIMU YA AWALI (ENGLISH MEDIUM) KWA MWAKA 2025/2026**

## 1.0 UTANGULIZI
Napenda kukupongeza na kukuarifu kuwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imekuchagua kujiunga na Mafunzo ya Ualimu ngazi ya Stashahada ya Ualimu Elimu ya awali **(English Medium).**

## 2.0 MAHALI CHUO KILIPO
Chuo Cha Ualimu Dakawa kipo **Mkoa wa Morogoro,** Wilaya ya Kilosa, Umbali wa kilometa **60** kutoka Morogoro Mjini, Barabara Kuu iendayo **Dodoma.** Ukifika **Msamvu, Morogoro** Stendi kuu ya mabasi**,** uliza stendi ya magari madogo (Daladala au Noah) yaendayo **DUMILA,** shuka njia panda ya **VETA Dakawa.** Pia, ukitokea Dodoma; Shuka njia panda ya **VETA Dakawa** kisha chukua usafiri wa pikipiki wakulete chuo cha Ualimu Dakawa, umbali wa kilometa nne (**4)** tu kutoka barabara kuu. Nauli ya pikipiki si zaidi ya **Tshs. 3,000/=.**

**NB:** Unashauriwa kufika mapema kabla ya saa 11:00 jioni kwa ajili ya usalama wako.

## 3.0 KUFUNGUA CHUO
Unatakiwa kufika chuoni tarehe **……………..** na mwisho wa kufika chuoni ni wiki mbili mara baada ya kufungua chuo bila kukosa**.** Utakapofika chuoni nenda **Ofisi ya Udahili, vyeti na mitihani** ambapo utapata maelekezo na taratibu zote za chuo na kusajiliwa.

**Kukamilisha usajili unatakiwa kuwa na vitu vifuatavyo:**

3.1 Barua ya kuitwa kujiunga na mafunzo ya Ualimu (Joining Instruction).
3.2 **Vyeti halisi vya Taaluma** (Original Academic Certificates) Kidato cha **nne,** Kidato cha **sita, cheti cha Astashahada Elimu ya Awali au Msingi** Au Hati ya matokeo (Result slip) kwa wale waliomaliza Kidato cha **Sita mwaka 2025** na **Astashahada Elimu ya Awali au Msingi mwaka 2025.**
3.3 Vyeti **halisi vya kuhitimu** (Leaving Certificates) Kidato cha **nne** na Kidato cha **sita.**
3.4 Cheti halisi cha kuzaliwa (original birth certificate).
3.5 Walioajiriwa walete barua za ruhusa ya kuhudhuria mafunzo kutoka kwa waajiri wao.
3.6 Uje pia na vivuli **(photocopies)** vinne vya vyeti vyako vyote.
3.7 Hakikisha umepimwa afya na Daktari wa Hospitali ya Serikali ya Wilaya (Fomu imeambatanishwa pamoja na barua hii).
3.8 Picha mbili za rangi (passport size).

3.9 Kadi ya BIMA YA AFYA vinginevyo uje na namba ya NIDA.

**NB: Kumbuka hutapokelewa chuoni iwapo hautawasilisha nyaraka tajwa hapo juu.**

## 4.0 ADA

Ada ya mafunzo Ualimu ni **TShs. 450,000/= kwa mwaka. Ada hii inaweza kulipwa yote kwa mkupuo au kwa awamu mbili Tsh. 225,000/=** kwa kila muhula. Ada italipwa kwa mtandao (GEPG) baada ya kutengenezewa namba ya malipo **(Control number)** na Mhasibu wa chuo kabla ya kufika chuoni kwa kuwasiliana na Mhasibu namba 0657104040. Fedha taslimu hazitapokelewa.

4.1 Utapaswa kulipa ada ya mtihani wa Taifa kiasi cha **Tsh. 50,000/=** (kwa mwaka wa II).

## 5.0 FEDHA YA MICHANGO

Utatakiwa kulipa Fedha ya Michango kwa ajili ya mahitaji mbalimbali kama inavyoonesha katika jedwali hapo chini;

| Na. | MCHANGO | KIASI | MAONI |
|---|---|---|---|
| 1 | Serikali ya wanachuo | 5,000/= | Kwa Mwaka |
| 2 | Huduma ya kwanza | 10,000/= | Kwa Mwaka |
| 3 | Usafi na mazingira | 20,000/= | Kwa Mwaka |
| 4 | Kukodisha godoro | 10,000/= | Kwa Mwaka |
| 5 | Usajili na Kitambulisho | 20,000/= | Kwa Mwaka wa kwanza tu |
| 6 | Michezo | 30,000/= | Kwa Mwaka |
| 7 | Ulinzi | 30,000/= | Kwa Mwaka |
| 8 | Ukarabati na Matengenezo | 25,000/= | Kwa Mwaka |
| 9 | Bima ya Afya Taifa | 50,400/= | Kwa wasio na Bima ya Afya (kwa mwaka) |
| 10 | Kukodi vazi la mahafali (Joho) | 15,000/= | Kwa mwaka wa pili tu |
| 11 | Mahafali | 20,000/= | Kila mwaka |
| | **JUMLA** | **235,400/=** | |

**NB:-**

Malipo ya fedha ya michango yote yafanyike kwenye Akaunti ya Chuo cha Ualimu Dakawa, Namba **01J1048471300; Jina la Akaunti ni: DAKAWA TC –SELF RELIANCE katika benki ya CRDB. Pia unaweza kulipia katika tawi lolote la CRDB nchini na wakala wake waliopo karibu nawe. Kisha uje na *BANK PAY IN SLIP*. Tafadhali usije na fedha taslimu ya Michango haitapokelewa.** Hakikisha unaandika jina la mwanachuo anayehusika na mafunzo katika risiti ya malipo hayo.

## 6.0 SARE YA CHUO

### 6.1 Wanaume

(a) Vazi rasmi la chuo ni **uniform pair** mbili. Suruali ya bluu nyeusi (darkblue) na nyeusi zenye marinda mawili yenye mkunjo chini (turn up) (**Rejea picha Na. 1**). Suruali nyeusi itavaliwa siku za jumatatu hadi jumatano na suruali ya buluu nyeusi itavaliwa siku za alhamisi na ijumaa. Aidha, koti la suti lenye mipasuo miwili nyuma na lenye rangi sawa na suruali litavaliwa na linaweza kuwa na kifungo kimoja au viwili (**Rejea picha Na. 5**). Suruali itavaliwa na mkanda mweusi.

(b) Mashati mawili (2) ya bluu bahari (light blue) mikono mirefu yanapatikana chuoni kwa bei ya **Tsh. 30,000/=** tu kwa yote mawili. Chuo kimeandaa utaratibu huu kuepusha kuwa na mashati ya rangi tofauti. Ukija na mashati yako hayatapokelewa.

(c) Tai ndefu buluu nyeusi (dark blue) au nyeusi. Tai itavaliwa kuendana na rangi ya suruali.

(d) Viatu vyeusi vya ngozi vya kutumbukiza (kufunika) kisigino kifupi. Viatu vitavaliwa na soksi ndefu nyeusi.

(e) T-shirt yenye nembo ya chuo rangi ya light blue **(Bluu Bahari)** inapatikana chuoni kwa bei ya **Tsh. 15,000/= tu**.

(f) Hairuhusiwi kuvalia suruali chini ya kiuno (mlegezo).

(g) Mwanachuo anapaswa kuwa na sare ya michezo ambayo ni tisheti nyeupe, 'track suit' ya bluu bahari, bukta ya buluu moja (1) na raba nyeupe. Sare ya michezo ivaliwe wakati wa michezo tu.

(h) Uvaaji wa jinzi, kaptula, bangili, cheni, vimodo, skafu, makobazi, vilaka, na pete (zisizo za ndoa) na vingine vinavyofanana na hivyo hauruhusiwi.

6.2 **Wanawake**

(a) Sketi mbili za rinda boksi ya bluu nyeusi (dark blue) na nyeusi zenye urefu unaozidi magoti inchi nne (4) na zisizobana (**Rejea picha Na. 2**). Sketi nyeusi itavaliwa siku za jumatatu hadi jumatano na sketi ya buluu nyeusi itavaliwa siku za alhamisi na ijumaa. Aidha, koti la suti lenye rangi sawa na rangi ya sketi litavaliwa (**Rejea picha Na. 4**).

(b) Mashati mawili (2) ya buluu bahari (light blue) mikono mirefu yanapatikana chuoni kwa bei ya **Tsh. 30,000/=** tu kwa yote mawili. Chuo kimeandaa utaratibu huu kuepusha kuwa na mashati ya rangi tofauti. Ukija na mashati yako hayatapokelewa.

(c) Tai ndefu 'dark blue' au nyeusi. Tai iendane na rangi ya sketi.

(d) Viatu vyeusi vya ngozi vya kutumbukiza kisigino kifupi (simple shoes haviruhusiwi), na soksi ndefu nyeupe.

(e) Nywele zichanwe au zisukwe mtindo wa utii wa roda (twende kilioni) mistari mitano (5) hadi nane (8) au kubanwa kisogoni kwa kibanio cheusi.

(f) Mwanachuo atakayependa kujisitiri kwa vazi la hijab anaelekezwa watumie rangi ya Light Blue **(Bluu Bahari)** (ifanane na shati) urefu usawa wa kifua.

(g) Mwanachuo anapaswa kuwa na sare ya michezo ambayo ni tisheti nyeupe, 'track suit' ya buluu bahari, bukta ya buluu moja (1) na raba nyeupe. Sare ya michezo ivaliwe tu wakati wa michezo.

(h) Uvaaji wa nguo angavu, khanga, kitenge, kofia, kilemba, hereni, bangili, mkufu, shanga, pensi, sketi fupi, nguo zenye mpasuo unaozidi magoti, makobazi na pete (isipokuwa pete ya ndoa) hauruhusiwi.

(i) T-shirt yenye nembo ya chuo rangi ya light blue **(Bluu Bahari)** inapatikana chuoni kwa bei ya **Tsh. 15,000/= tu**.

**NB**: HAKIKISHA UNAVAA nguo za michezo, tracksuit ya buluu bahari (**'light blue' na raba nyeupe)** siku ya kuja kuripoti chuoni ili kutokuathiri kupokelewa chuoni.

## 7.0 VIFAA/MAHITAJI MENGINE MUHIMU

7.1 Blanketi, shuka mbili za light blue na foronya za light blue, mto pamoja na chandarua kwa ajili

ya kujikinga na mbu.

7.2 Vyombo vya chakula kama vile sahani, bakuli, kikombe **(visiwe vya plastic),** kijiko, galoni ya plastiki ya lita 5 ya kuhifadhia maji yako ya kunywa.

*7.3* Ndoo ya kuogea. (*Hupatikana pia katika maduka yaliyopo karibu na chuo)*

7.4 Tochi yenye betri kwa ajili ya tahadhari ya kukosekana kwa umeme.

7.5 Pazia **Light blue** urefu wa ft. 9 kwa ft. 3.5 kwa ajili ya chumba chako.

7.6 Daftari kubwa zisizopungua 10 kwa muhula (Counter book Quare 2) (hupatikana pia katika maduka yaliyopo karibu na chuo.


7.7 Vitabu mbalimbali na Mihtasari ya masomo yako uliyochaguliwa.

*7.8* Rimu moja ya karatasi nyeupe (A4 photocopy paper) kwa ajili ya shughuli za kitaaluma. Hii hutolewa kila mwaka wa masomo. *(Hupatikana pia katika maduka yaliyopo karibu na chuo).*


7.9 Uje na ‘’scientific calculator’’ kwa ajili ya somo la upimaji na tathmini.

7.10 Elimu bora hutolewa katika mazingira safi na salama. Hivyo basi, **wanaume** wanapaswa kuleta **reki (imara) moja** na **wanawake** wanapaswa kuleta **fyekeo/kwanja (imara) moja.** Vifaa hivi mtavitumia kufanyia usafi katika mazingira ya chuo.

**MAVAZI KWA WANACHUO**



**Picha Na.1**




**Picha Na. 2**



**Picha Na. 3**



**Picha Na. 4**



**Picha Na.5**

8.0 **MAAGIZO MUHIMU KWA AJILI YA WANACHUO**

(a) Unashauriwa kuja na sanduku imara lenye kufuli kwa utunzaji salama wa vifaa vyako.
(b) Unashauriwa kuja na rimu moja kwa ajili ya matumizi yako binafsi.
(c) Unashauriwa kuja na fedha taslimu kwa ajili ya matumizi binafsi.
(d) Unashauriwa kuja na mavazi mengine mbali ya sare ila yawe ya mashono ya Heshima na yanayoakisi Taaluma ya Ualimu (Mavazi hayo yatakaguliwa ofisi ya udahili).

9.0 **MWISHO:**

Mwanachuo ambaye hatakamilsha maagizo yote, hatapokelewa/sajiliwa. Tafadhali, siku ya kuripoti chuoni vaa **full tracksuit ya bluu bahari** (**light blue)** na raba nyeupe za michezo ili upokelewe.

Katika kipindi chote cha mafunzo, mwanachuo atatakiwa kutii sheria za Nchi, za Chuo na Kanuni za mwenendo bora wa mwanachuo. Ufikapo chuoni utakabidhiwa nakala ya Sheria, Kanuni na Taratibu za Chuo. Pia utatakiwa kukiri au kukubali nafasi hiyo ya mafunzo kwa kujaza fomu.

"***Ualimu bora huanzia chuoni, tunakutegemea kuwa Mwalimu bora tangu mwanzo wa mafunzo yako"***

**KARIBU SANA CHUO CHA UALIMU DAKAWA**

__________________________

**DOROTHY I. MHAIKI**
**MKUU WA CHUO**

**Kwa Mawasiliano:**

**0767259510** Mkuu wa Chuo
**0714471818** Makamu Mkuu wa Chuo
**0657104040** Mhasibu
**0658553773** Mkuu wa Idara ya Udahili

**Nakala:** Mkurugenzi Elimu ya Ualimu,
Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia,
S .L .P .10
**40479 DODOMA**

## GOVERNMENT OF TANZANIA
## REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

**PART A**

**To:**
**The Medical Officer**
…………………………………………………..
…………………………………………………...
…………………………………………………..

Mr/Mrs/Miss ………………………………………………………………………………
(Name in full)

Please examine the above named as to his/her physical and mental fitness for a full time teacher training course.
The examination should include the following categories (i – ii) each category or sub category of which will render the applicant ineligible in case of a defect.

Primary/category iv will also render a girl candidate ineligible for the course:-

(i) (a) Eye-sight (b) Hearing (c) Limbs (d) Speech
(e) Venereal disease (f) Leprosy (g) Epilepsy
(ii) Neuroses
(iii) Other serious diseases
(iv) Pregnancy

**MEDICAL CERTIFICATE**

**PART B:** (To be completed by a Government Medical Officer)

I have examined the above named and consider that he/she is physical fit/unfit and mentally fit/unfit for a full time teacher training course.

(i) (a) Eye-sight………………… (b)Hearing………………(c)Limbs ………………………
(d) Speech………………….. (e) Venereal diseases……………………………………
(f) Leprosy ………………….. (g) Epilepsy……………………………………………..
(ii) Neuroses ……………………….............................................................................
(iii) Serious diseases…………………………………………………………………………
(iv) Pregnancy…………………………………………………………………………

**Date** ………………………………………… **Signature** ………………………………………

**Station** ……………………………………… **Designation** ……………………………………